# Lipia kawi yako pesa kidogo

## Kwa programu ya PGE ya Kipunguzo cha bili ya Mapato Yaliyofuzu

Mpango wetu wa Income-Qualified Bill Discount (Punguzo la Bili kwa Wenye Kipato Kinachostahili) ni njia bora kabisa ya kupata punguzo la kila mwezi la kati ya 15% na 60% kwenye matumizi yako ya nishati* na ni rahisi kutuma maombi!

1. **Usaidizi wa bili** unaoendelea kila mwezi Kipunguzo hiki cha kila mwezi kinachoendelea ni cha kuongezea usaidizi wowote mwingine ambao huenda unapokea kutoka kwetu au mashirika mengine.

2. **Huenda tayari unafuzu** Kutegemea ukubwa wa kaya yako na mapato ya kila mwaka, kipunguzo chako cha kila mwezi kinaweza kuwa kati ya 15% na 60%. Kwa yote, iwapo umepokea usaidizi wa kawi katika siku zilizopita, huenda tayari umefuzu.

3. **Usajili wa urahisi** Hatutahitaji hati zozote za kifedha kutoka kwako ili utume ombi. Tutahitaji tu kujua ukubwa wa kaya yako na jumla ya mapato ya kaya yako kwa mwaka.

4. **Ni rahisi kutuma ombi** Washauri wetu wa Huduma kwa Mteja anaweza kukusaidia katika zaidi ya lugha 200. Tupigie tu simu kupitia 503-228-6322 na tutakuelezea kila kitu. Au jaza fomu rahisi na ama utume kwa barua au upakie katika **portlandgeneral.com/formupload** (tazama maagizo kwenye fomu ya ombi).

## Je, unafuzu? Acha tujue!

Usajili unapatikana kwa wateja wakaazi wanaopatikana wa Portland General Electric (PGE, Umeme wa Jumla wa Portland). Ustahiki unategemea ukubwa wa kaya yako na jumla ya mapato ya wastani kwa mwaka kwa wanachama wote wa kaya yako walio na umri wa miaka 18 na zaidi. Jumla ya mapato inamaanisha mapato ya kaya yako kabla ya ushuru.

Ifuatayo ni miongozo iliyopangwa kutegemea ukubwa na mapato ya kaya.

| Ukubwa wa kaya | Mapato ya jumla ya kila mwezi** | Mapato ya jumla kila mwaka ya kaya** |
|---|---|---|
| 1 | $3,067.58 | $36,811 |
| 2 | $4,011.50 | $48,138 |
| 3 | $4,955.33 | $59,464 |
| 4 | $5,899.17 | $70,790 |
| 5 | $6,843.08 | $82,117 |
| 6 | $7,786.92 | $93,443 |
| 7 | $7,963.92 | $95,567 |
| 8 | $8,140.83 | $97,690 |
| 9 | $8,317.83 | $99,814 |
| 10 | $8,494.83 | $101,938 |
| 11 | $8,671.83 | $104,062 |
| 12 | $8,848.75 | $106,185 |
| Kila mwanachama wa ziada | $176.92 | $2,123 |

**Mapato ya jumla inamaanisha mapato yote ya kaya yako kabla ya makato yoyote.

Viwango hivi vinategemea mapato ya jumla kwa mwaka ya kaya katika au chini ya 60% ya Mapato ya Wastani ya Jimbo (SMI) kufikia Oktoba 2024. Miongozi hii husasishwa kila mwaka.

Iwapo una maswali kuhusu kupiga hesabu ya mapato yako, mahitaji ya programu, au unahitaji usaidizi wa kutuma ombi, tupigie simu kupitia **503-228-6322**. Tuko hapa kusaidia.

*Kipunguzo hiki hakitumiki kwa jumla ya kiwango unachodaiwa kwa mwezi. Gharama fulani hazijajumuishwa katika kipunguzo.

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

Utapata maelezo zaidi ya programu katika portlandgeneral.com/pgediscount (katika Kiingereza). Washauri wetu wa Huduma kwa Mteja pia wanaweza kukusaidia katika zaidi ya lugha 200 kupitia 503-228-6322.

## PGE hufanya nini na mapato yangu na taarifa ya kaya?

- Taarifa yako imelindwa. Tunatumia tu taarifa ya mapato na ya kaya yako ili kuthibitisha kuwa unastahiki kupata programu hii.

## Je, na iwapo ukubwa wa kaya yangu au mapato yangu hubadilika?

- Iwapo ukubwa wa kaya yako au mapato yako yatabadilika, utahitaji kuwasilisha fomu mpya kupitia barua, kuipakia mtandaoni au kutupigia simu na kutuambia taarifa yako mpya.

## Je, kukuwa katika programu ya Kipunguzo cha bili ya Mapato Yaliyofuzu kutaathiri uwezo wangu wa kupokea usaidizi wa kawi?

- La. Programu hizi ni tofauti na kupokea usaidizi wa kawi hakutaathiri uwezo wako wa kujisajili katika kipunguzo cha bili ya PGE. Mara tu umejisajili katika programu ya kipunguzo, bado unaweza kutuma ombi na kupokea usaidizi wa kawi.

## Nafaa kutarajia nini baada ya kujisajili?

- Mara tu umewasilisha fomu yako kupitia barua au mtandaoni, au kutupigia simu ili kujisajili, tutakagua maelezo yako ili kuona kama unafuzu kuingia kwenye programu hii. Tafadhali ruhusu siku 30 zipite ili ombi lako lichakatwe.
- Mara tu umeidhinishwa, tutakutumia barua pepe au barua ya kukuarifu ili kuthibitisha usajili wako na asilimia ya kipunguzo utakachopokea.
- Kwa msingi wa kila mwaka, tutauliza idadi ndogo ya wateja waliosajiliwa kutoa idhibati ya ukubwa wa kaya na mapato ili kuhakikisha kuwa wateja wanastahiki.

## Iwapo nafuzu, ni nini tena nafaa kujua kuhusu programu hii?

- Mara tu umejisajili, kipunguzo cha kila mwezi kitadumu kwa miaka miwili. Utahitaji kujisajili tena baada ya miaka miwili, lakini tutakutumia kikumbusho mapema. Kipunguzo kinatumika tu kwa gharama mpya zilizotumwa baada ya usajili. Kipunguzo hiki hakitumiki kwa gharama zilizotumwa kabla ya kujisajili.
- Kipunguzo hiki kitatumika kwa bili ya kwanza utakayopokea baada ya usajili wako kuidhinishwa.
- Kipunguzo hiki hakitumiki kwa jumla ya kiwango unachodaiwa kwa mwezi. Gharama fulani hazijajumuishwa katika kipunguzo.

## Ni nini kinazingatiwa au hakizingatiwi kama mapato?

- Angalia jedwali linalofuata kwa mifano ya kawaida ya kinachozingatiwa na kisichozingatiwa kama mapato.

**Hiki kinazingatiwa kama mapato**

- Masurufu
- Malipomwaka
- Msaada wa mtoto
- Faida
- Mshahara uliopata
- Malipo ya wanaoishi na mtoto
- Malipo ya jeshi
- Pensheni
- Mrabaha
- Mapato ya mtu anayefanya kazi yake (baada ya matumizi)
- Social Security (Usalama wa Umma)
- Social Security Disability (Ulemavu wa Usalama wa Umma, SSDI)
- Supplemental Security Income (Mapato ya Ziada ya Usalama, SSI)
- TANF
- Ukosefu wa Ajira

**Hiki hakizingatiwi kama mapato**

- Usaidizi wa Kawi
- Mapato ya watu walio katika shule ya upili au chini ya miaka 18
- Marejesho/mikopo ya ushuru wa mapato
- Zawadi za pesa ya mara moja
- Rehani ya kurejeshewa
- Sehemu 8 au misaada ya nyumba
- Marupurupu ya matumizi
- Manufaa ya Women, Infants and Children (WIC, Wanawake, watoto wachanga na Watoto)

→ Mbali na mpango wa PGE's Income-Qualified Bill Discount, pia unaweza kustahiki kupata usaidizi kutoka kwa NW Natural, Pacific Power au Xfinity. Pata maelezo zaidi kupitia nwnatural.com/billdiscount, Pacificpower.net/LID au xfinity.com/internetessentials.

**Changanua msimbo wa QR kupata toleo la kidijitali la maombi haya.**

PGE

# Ombi la Kipunguzo cha Bili ya Mapato Yaliyofuzu

*Tumia fomu hii katika ombi lako la awali au kusasisha taarifa yako iwapo ukubwa au mapato ya kaya yako yatabadilika.*

**Jina la kwanza na la mwisho Portland General Electric** (PGE, jina la msingi kwenye bili yako ya)

**Namabri ya akaunti ya PGE** (dijiti 10)

**Anwani ya huduma** (makao ya msingi)

**Anwani ya barua pepe**

**Nambari ya simu ya unayopendelea**

**Lugha unayopendelea**

*Washauri wetu wa Huduma kwa Mteja anaweza kukusaidia katika zaidi ya lugha 200. Pia unaweza kuomba kwa kutupigia simu kupitia 503-228-6322.*

**Je, mtu katika kaya yako ana mahitaji ya matibabu yanayohitaji umeme?** Iwapo tayari hujajisajili, tutafuatilia na wewe ili kushiriki taarifa kuhusu [programu yetu ya Cheti cha Matibabu] (katika Kiingereza).

☐ Ndiyo

☐ La

## Taarifa ya kaya na mapato

Kipunguzo chako kitategemea ukubwa wa kaya yako na wastani ya jumla ya mapato ya kaya yako kila mwaka (kabla ya ushuru).

**Ukubwa wa kaya** (wanachama wote wakiwemo watu wazima na watoto)

$ **Jumla ya wastani ya mapato ya kila mwaka ya kaya yangu**

**Je, unahitaji usaidizi wa kupiga hesabu ya mapato yako? Pata vidokezo kwenye ukurasa wa pili.**

☐ Kwa sasa napokea mapato yasiyobadilika na napokea mapato au manufaa kutoka kwa moja au zaidi ya yafuatayo: Usalama wa Umma, State Supplementary Payment (SSP, Malipo ya Ziada ta Taifa) au Social Security Disability (SSDI, Ulemavu wa Usalama wa Kijamii) mapendeleo/gawio la akaunti za kustaafu, Medicaid au Supplemental Security Income (SSI, Mapato ya Usalama wa Ziada)

# Jinsi ya kupiga hesabu ya mapato ya kila mwaka ya kaya yako

Kwa wafanyakazi ambao hulipwa kwa saa walizofanya kazi, chukua marupurupu ya kila saa na kujumlisha na wastani wa jumla ya saa ulizofanya kazi kila wiki. Kisha jumlisha nambari hiyo na 52 (wiki kwa mwaka) ili kupata jumla ya mapato yako ya kila mwaka (kabla ya ushuru).

Iwapo mapato ya kaya yako hubadilika kila mwezi, chukua jumla ya mapato yako kutoka mwezi jana na kujumlisha na 12 ili kupiga hesabu ya wastani wa jumla ya mapato ya kila mwaka ya kaya yako.

Iwapo una maswali yoyote kuhusu kupiga hesabu ya mapato yako, mahitaji ya programu, au unahitaji usaidizi wa kutuma ombi, tupigie simu kupitia **503-228-6322**. Tuko hapa kusaidia.

**Mfano:**

**$13.50** *(kiwango cha kila saa)*
**x 40** *(wastani ya saa ulizofanya kazi kwa wiki)*
**= $540**

**$540**
**x 52** *(wiki kwa mwaka)*
**= $28,080**
*(Haya ndiyo jumla ya mapato yako kwa mwaka.)*

## Azimio

- Nafahamu kuwa hii ni ombi la kwanza na PGE itafuatilia na mimi baada ya usajili wa kawaida kwa maelezo kuhusu kipunguzo changu.
- Nitaarifu PGE iwapo jumla ya mapato yangu ya kila mwaka au ukubwa wa kaya hubadilika kwa kuwasilisha ombi jipya mtandaoni au kwa kupigia PGE simu kupitia **503-228-6322** ili maelezo yangu yaweze kusasishwa.
- Nafahamu kuwa naweza kuhitajika kutoa uthibitisho wa mapato ya kaya na ukubwa wa kaya nikiulizwa. Taarifa litapatikana kwa PGE na watu au taasisi zinazofanya kazi kwa niaba ya PGE kutekeleza programu hii.
- Nafahamu kuwa kipunguzo hiki hakitatumika kwa gharama zangu za awali, lakini gharama mpya pekee zilizotozwa baada ya usajili (usajili unaweza kuchukua hadi siku 30) na si jumla ya kiwango kinachodaiwa kwenye bili. Gharama fulani hazijajumuishwa katika kipunguzo hiki.

Kwa kusaini azimio hili, nathibitisha kuwa taarifa ambayo nimetoa katika ombi hili ni kweli na sahihi. Nakiri kuwa nimesoma na kufahamu maudhui ya ombi hili. Pia nakubaliana na sheria na masharti yaliyobainishwa katika Orodha ya Bei ya PGE Kipunguzo cha Bili ya Mapato Yanayofuzu katika **portlandgeneral.com/iqbdtariff** (katika Kiingereza).

**Saini ya kielektroniki** (tafadhali weka jina lako kamili)

## Demografia

Swali linalofuata ni la hiari na halitumiki katika ustahiki lakini litahakikisha kuwa tunawahudumia wateja wetu kwa usawa. Ipi kati ya zifuatazo inakufafanua bora?

- ☐ Mwafrika Mhamiaji au Mkimbizi
- ☐ Mwasia au Mhindi Mwasia
- ☐ Mmarekani Mweusi au Mwafrika
- ☐ Mlatino, Mhispanyola, au Mhispania
- ☐ Mwasili wa Mashariki ya Kati
- ☐ Mmarekani Asili na/au Mwasili wa Alaska
- ☐ Mwasili wa Hawaii na/au Mwasili wa Kisiwa cha Pasifiki
- ☐ Mslavia
- ☐ Mzungu au Mkokasia
- ☐ Nyingine: ____________
- ☐ Napendelea kutojibu

**Uko tayari kuwasilisha?** Pakia ombi lako lililokamilishwa katika **portlandgeneral.com/formupload** au tuma kama barua kwa **PGE Bill Discount, 7895 SW Mohawk St., Tualatin, OR 97062**.

127106 SWA (5/25)